

Februari 28, 2023

# JARIDA LA KOROSHO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA KILIMO  
BODI YA KOROSHO TANZANIA



Toleo  
la  
Februari

2023

[www.cashew.go.tz](http://www.cashew.go.tz)



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA KILIMO BODI YA KOROSHO TANZANIA



Februari 28, 2023 [www.cashew.go.tz](http://www.cashew.go.tz)

## 1.0 UTANGULIZI

Msimu wa Korosho nchini Tanzania huanza mwezi Oktoba na kuisha mwezi wa Aprili, hii ni baada ya mikoa mipyka kuanza kuzalisha korosho. Hata hivyo zaidi ya asilimia 90 ya korosho ghafi huzalishwa katika Mikoa ya kusini mwa Tanzania ambayo ni Mtwara, Lindi, Ruvuma na Pwani ambayo msimu wake ni kuanzia Oktoba hadi Mwezi Januari. Mpaka sasa minada katika mikoa hiyo tayari imesitishwa. Kiasi kidogo cha korosho zilizobaki zinaendelea kuuzwa kwa wabanguaji wa ndani kupitia Soko la awali. Kwa upande wa kanda ya Kaskazini na kanda ya kati, hususani mikoa ya Tanga, Dodoma na Singida tayari imeanza mavuno ambapo msimu wake huanza mwezi wa Februari hadi Aprili. Mpaka sasa mkoa wa Tanga tayari umeshafanya mnada wa kwanza tarehe mosi mwezi Februari na minada hiyo itaendelea hadi mwezi Aprili kulingana na upatikanaji wa korosho. Mikoa ya Dodoma na Singida inatarajia kuanza minada mwezi Machi. Shughuli ya utoaji wa vibali vya kusafirisha Korosho ghafi nje ya nchi inaendelea ambapo hadi sasa zaidi ya tani 169,238.720 za korosho ghafi zimeombewa vibali vya kusafirisha nje ya nchi. Pia vibali vya kusafirisha korosho karanga vinaendelea kutolewa na hadi sasa zaidi ya tani 1,441.140 zimesafirishwa. Kulingana na kalenda ya mwaka ya zao la korosho, kipindi hiki ni muda wa kupanda mbegu, kupandikiza miche bora na kupanda mazao mchanganyiko ili kurahissha palizi.

## 2.0. MWENENDO WA SOKO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI

### 2.1. MWENENDO WA SOKO AFRIKA MAGHARIBI

Nchini Ivory Coast sherehe za ufunguzi wa msimu zilitarajiwa kufanyika tarehe 27 Februari, 2023 na bei elekezi ya korosho ghafi ni kati ya Dola za Kimarekani 1,280 hadi 1,300 kwa tani.

Kwa upande wa nchi ya Ghana msimu mipyka tayari umeanza na bei ya korosho ghafi inakadirwa kuwa Dola za Kimarekani 1,300 kwa tani kwa korosho zenye ubora wa "50-51 lbs" na bei ya Dola za Kimarekani 1,325 kwa tani korosho zenye ubora wa "52 lbs" kwa soko la India.

Nchini Benin msimu wa ma mauzo ya korosho ghafi utazinduliwa rasmi tarehe 09 Machi, 2023.

Huku nchini Nigeria tayari msimu wa mauzo umeanza na wastani wa bei ni Dola za Kimarekani 1,175 hadi 1,180 kwa tani kwa korosho zenye ubora wa "50 lbs" kwa soko la India na Dola za Kimarekani 1,300 kwa korosho zenye ubora wa "51-52 lbs".

### 2.2. Hali ya Soko la Korosho Nchini India

Bei ya korosho karanga inaendelea kuwa thabiti. Mahitaji ya korosho ghafi bado yanaonekana ni makubwa hasa kwa kuangalia takwimu za misimu mitatu.


## Jedwali Na.1: Hali ya Uzalishaji/Biashara ya Korosho Nchini India.

| Haliya Uzalishaji/Biashara ya Korosho Nchini India (Milioni za Tani "000000") |                     |                              |                   |                            |                      |                                     |
|---|---------------------|------------------------------|-------------------|----------------------------|----------------------|-------------------------------------|
| Mwaka   | Uzalishaji wa Ndani | Uagizaji kuto ka Nje (Ghafi) | Jumla ya Mahitaji | Uzalishaji Korosho Karanga | Usafirishaji Korosho | Matumizi ya Ndani (Korosho Karanga) |
| 2019-2020   | 0.700               | 0.910                        | 1.620             | 0.310                      | 0.084                | 0.223                               |
| 2020-2021   | 0.738               | 0.838                        | 1.572             | 0.319                      | 0.070                | 0.249                               |
| 2021-2022   | 0.750               | 0.950                        | 1.700             | 0.322                      | 0.052                | 0.270                               |

Note: Wastani wa Bei ya Korosho Ghafi ni Dola za Kimarekani 1.08 kwa Kilogramu

Chanzo: Cashewnutinformation 23-25 Feb 2023

Hali ya Biashara ya Korosho India (Kwa Milioni za Tani)



## 2.3. Hali ya Soko la Korosho katika Nchi ya Vietnam


Bado kuna uhitaji mkubwa wa korosho ghafi kwa wabanguaji wadogo, na hii inapelekea bei ya korosho ghafi kwa soko la ndani kuwa kubwa ukilinganisha na msimu uliopita.

Kwa siku za hivi karibuni mahitaji ya korosho karanga ni hafifu, wanunuzi wanahisi bei ya korosho karanga itashuka kutokana na kuanza kwa msimu wa mauzo ya korosho ghafi katika nchi za Afrika Magharibi na Cambodia ambapo sehemu kubwa ya korosho ghafi zitauzwa nchini Vietnam.

## Jedwali Na.2: Bei za Korosho Ghafi katika Nchi ya India na Vietnam Februari, 2023

| MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI (RCN)<br>DUNIANI-CASE STUDY YA INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI<br>CHA OKTOBA, 2022 HADI FEBRUARI, 2023 |                 |            |
|---|-----------------|------------|
| TAREHE  | BEI-CIF USD/TON |            |
|   | BEI YA CHINI    | BEI YA JUU |
| 02 Oktoba, 2022   | 1,080           | 1,350      |
| 31 Oktoba, 2022   | 1,050           | 1,280      |
| 05 Novemba, 2022  | 1,100           | 1,400      |
| 27 Novemba, 2022  | 1,100           | 1,400      |
| 12 Desemba, 2022  | 1,100           | 1,330      |
| 24 Desemba, 2022  | 1,150           | 1,320      |
| 14 Januari, 2023  | 1,200           | 1,275      |
| 28 Januari, 2023  | 1,250           | 1,390      |
| 18 Februari, 2023   | 1,180           | 1,230      |
| SOT: 49-52  |                 |            |

Mwenendo wa Bei Katika Nchi ya India na Vietnam Hadi Februari, 2023



Chanzo: Cashewnutinformation

### 3.0 BEI YA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

#### 3.1 Bei ya Korosho Karanga Vietnam Kufikia Februari, 2023

Nchini Vietnam bei ya korosho karanga iko chini ukilinganisha na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Kuna mabadiliko madogo ya bei kwa mwezi Februari kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3

##### Jedwali Na. 3

| BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 |        |                     |            |                    |            |
|--|--------|---------------------|------------|--------------------|------------|
| MAELEZO YA DARAJA  | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) |            | Bei TZS/Kilo (FOB) |            |
|  |        | Bei ya Chini        | Bei ya Juu | Bei ya Chini       | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180                                    | WW180  | 7.28                | 7.50       | 16,896.88          | 17,407.50  |
| White Whole Cashews 210                                    | WW210  | 6.73                | 6.95       | 15,620.33          | 16,130.95  |
| White Whole Cashews 240                                    | WW240  | 5.84                | 6.17       | 13,554.64          | 14,320.57  |
| White Whole Cashews 320                                    | WW320  | 5.47                | 5.73       | 12,695.87          | 13,299.33  |
| Large Pieces   | LP     | 3.31                | 3.86       | 7,682.51           | 8,959.06   |
| Small Pieces   | SP     | 2.76                | 2.98       | 6,405.96           | 6,916.58   |

##### Chanzo: Cashewinformation

#### 3.3 Bei ya Korosho Karanga katika nchi za Afrika Magharibi Hadi Kufikia Februari, 2023

Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni Ivory Coast, Ghana, Benin nk. Inakadiriwa kuwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 4

##### Jedwali Na. 4

| BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA FEBRURI, 2023 |        |                     |            |                    |            |
|--|--------|---------------------|------------|--------------------|------------|
| MAELEZO YA DARAJA  | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) |            | Bei TZS/Kilo (FOB) |            |
|  |        | Bei ya Chini        | Bei ya Juu | Bei ya Chini       | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180  | W180   |                     |            |                    |            |
| White Whole Cashews 210  | W210   | 8.16                | 8.49       | 18,939.36          | 19,705.29  |
| White Whole Cashews 240  | W240   | 5.95                | 6.28       | 13,809.95          | 14,575.88  |
| White Whole Cashews 320  | W320   | 5.73                | 5.95       | 13,299.33          | 13,809.95  |
| White Whole Cashews 450  | W450   | 5.29                | 5.62       | 12,278.09          | 13,044.02  |
| White Splits   | WS     | 4.52                | 4.96       | 10,490.92          | 11,512.16  |
| Large Pieces   | LP     | 3.86                | 4.41       | 8,959.06           | 10,235.61  |
| Small Pieces   | SP     | 3.09                | 3.42       | 7,171.89           | 7,937.82   |

##### Chanzo: Cashewinformation

### 3.4 Bei ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje ya Nchi Hadi Kufikia Februari, 2023

Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje kwa nchi za Uholanzi, Uturuki, Misri, nchi za Uarabuni nk. Ni kama ilivyo katika jedwali Na. 5

#### Jedwali Na. 5


| BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 |        |                     |            |                    |            |
|--|--------|---------------------|------------|--------------------|------------|
| MAELEZO YA DARAJA  | DARAJA | Bei Dola/Kilo (FOB) |            | Bei TZS/Kilo (FOB) |            |
|  |        | Bei ya Chini        | Bei ya Juu | Bei ya Chini       | Bei ya Juu |
| White Whole Cashews 180  | W180   | 7.97                | 8.37       | 18,486.00          | 19,422.00  |
| White Whole Cashews 240  | W240   | 7.36                | 7.56       | 17,082.00          | 17,550.00  |
| White Whole Cashews 320  | W320   | 6.96                | 7.26       | 16,146.00          | 16,848.00  |
| White Splits   | WS     | 3.93                | 4.54       | 9,126.00           | 10,530.00  |
| Large White Pieces   | LWP    | 3.93                | 4.54       | 9,126.00           | 10,530.00  |

Chanzo: TACP

#### Jedwali Namba 6: Uwiano Wa Bei Daraja WW320

| UWIANO WABEI DARAJA LA WW320 FOB |                        |                      |                       |                     |
|----------------------------------|------------------------|----------------------|-----------------------|---------------------|
| Nchi                             | Bei ya Chini Dola/Kilo | Bei ya Juu Dola/Kilo | Bei ya Chini TZS/Kilo | Bei ya Juu TZS/Kilo |
| Vietnam                          | 5.47                   | 5.73                 | 12,695.87             | 13,299.33           |
| Afrika Magharibi                 | 5.73                   | 5.95                 | 13,299.33             | 13,809.95           |
| Tanzania                         | 6.96                   | 7.26                 | 16,146.00             | 16,848.00           |

Uwiano wa Bei Daraja WW320 FOB



### 4.0 MWENENDO WA SOKO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2023 uzalishaji wa korosho ghafi kwa msimu wa 2022/2023 ni tani 182,960.784; ambapo tani 176,120.913 zimekusanya na kuuzwa katika ghala za minada zenye thamani ya shilingi 327,448,291,921. Bei ya chini kwa mwezi Februari, imepanda kwa asilimia 15.2 ikilinganishwa na mwezi Januari, 2023 ambapo bei ya chini ilikuwa 1,520 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya shilingi 1,751 kwa kilo mwezi Februari. Bei ya juu imeshuka kwa asilimia 1.1 mwezi Januari, 2023 ambapo bei ya juu mwezi Februari ilikuwa Tshs 1,770 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya shilingi 1,751 kwa kilo mwezi Februari. Mauzo ya korosho kupitia soko la awali hadi kufikia wiki ya mwisho ya mwezi wa Februari ni tani 3,199.412 na korosho zilizobanguliwa na wabanguaji wadogo ni takribani tani 808.991 sawa na tani 3,640.459 za korosho ghafi. Ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji unaendelea.

**Jedwali Na. 7a: Taarifa ya Uzalishaji Korosho Msimu wa 2022/2023 hadi Kufikia Mwezi Februari, 2023**

| TAARIFA YA UZALISHAJI KOROSHO MSIMU WA 2022/2023 |                |                     |                    |                      |                |
|--|----------------|---------------------|--------------------|----------------------|----------------|
| MKOA   | CHAMA KIKUU    | GHALA ZA MNADA (KG) | SOKO LA AWALI (KG) | ZILIZOBANGULIWA (KG) |                |
|  |                |                     |                    | ZILIZOBANGULIWA      | UWANO WA GHAFI |
| MTWARA   | TANECU         | 33,062,163.00       | 1,493,914.00       | 498,206.00           | 2,241,927.00   |
|  | MAMCU          | 59,609,668.00       | 1,235,822.00       | 119,185.00           | 536,332.50     |
| LINDI  | RUNALI         | 42,440,859.00       |                    |                      |                |
|  | LINDI MWAMBBAO | 14,622,801.00       | 322,442.00         | 191,600.00           | 862,200.00     |
| RUVUMA   | TAMCU          | 15,272,789.00       | 26,480.00          |                      |                |
| PWANI  | CORECU         | 10,759,506.00       | 89,581.00          |                      |                |
| TANGA  | TACACU         | 199,168.00          |                    |                      |                |
| SINGIDA  | CEAMCU         |                     | 18,769.00          |                      |                |
| MOROGORO   | UKICU          | 153,959.00          |                    |                      |                |
| TABORA   |                |                     | 2,000.00           |                      |                |
| KATAVI   |                |                     |                    |                      |                |
| MBEYA  |                |                     | 404.00             |                      |                |
| KIGOMA   |                |                     | 10,000.00          |                      |                |
| JUMLA NDOGO                                      |                | 176,120,913.00      | 3,199,412.00       | 808,991.00           | 3,640,459.50   |
| JUMLA KUU  |                |                     |                    |                      | 182,960,784.50 |

NB: Taarifa hii ya uzalishaji ni hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2023. Ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji bado unaendelea.

**Jedwali Na. 7b: Korosho Zilizouzwa Kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani.**

| Jumla ya Kiasi Kilichouzwa na Thamani (Februari, 2023) |                        |                 |
|--|------------------------|-----------------|
| KIPINDI CHA  | KIASI KILICHOUZWA (KG) | THAMANI (TZS)   |
| Mwezi Februari   | 199,168                | 335,185,568     |
| Jumlishi Oktoba-Januari                                | 175,921,745            | 327,113,106,353 |
| Jumla  | 176,120,913            | 327,448,291,921 |

**Jedwali Na. 7c: Muhtasari Bei za Korosho Ghafi Katika Minada**

| Muhtasari Bei za Korosho Ghafi Katika Mnada |                       |                                |              |
|---|-----------------------|--------------------------------|--------------|
| Mwezi Uliopita (Januari, 2023)              |                       | Mwezi wa Sasa (Februari, 2023) |              |
| Mwenendo wa Bei                             | Mwezi                 | Daraja la Kawaida              |              |
|   |                       | Bei ya Juu                     | Bei ya Chini |
|   | Bei ya Mwezi Februari | 1,751                          | 1,751        |
|   | Bei ya Mwezi Januari  | 1,770                          | 1,520        |
| Mabadiliko (%)                              |                       | ▼ 1.1%                         | ▲ 15.2%      |

## Jedwali Na. 7d: Bei za Mauzo ya Korosho Ghafi Kimkoa.

| Bei ya Mauzo Korosho Ghafi ya Mkao (Februari, 2023) |                |                       |                   |              |
|---|----------------|-----------------------|-------------------|--------------|
| MKOA  | CHAMA KIKUU    | MWEZI                 | Daraja la Kawaida |              |
|   |                |                       | Bei ya Juu        | Bei ya Chini |
| MTWARA  | MAMCU          | Bei ya Mwezi Februari | NA                | NA           |
|   |                | Bei ya Mwezi Januari  | 1,705             | 1,680        |
|   |                | Mabadiliko (%)        |                   |              |
|   | TANECU         | Bei ya Mwezi Februari | NA                | NA           |
|   |                | Bei ya Mwezi Januari  | 1,605             | 1,604        |
|   |                | Mabadiliko (%)        |                   |              |
| LINDI   | RUNALI         | Bei ya Mwezi Februari | NA                | NA           |
|   |                | Bei ya Mwezi Januari  | 1,770             | 1,600        |
|   |                | Mabadiliko (%)        |                   |              |
|   | LINDI MWAMBAAO | Bei ya Mwezi Februari | NA                | NA           |
|   |                | Bei ya Mwezi Januari  | 1,726             | 1,726        |
|   |                | Mabadiliko (%)        |                   |              |
| PWANI   | CORECU         | Bei ya Mwezi Februari | NA                | NA           |
|   |                | Bei ya Mwezi Januari  | 1,520             | 1,520        |
|   |                | Mabadiliko (%)        |                   |              |
| RUVUMA  | TAMCU          | Bei ya Mwezi Februari | NA                | NA           |
|   |                | Bei ya Mwezi Januari  | 1,605             | 1,605        |
|   |                | Mabadiliko (%)        |                   |              |
| MOROGORO  | UKICU          | Bei ya Mwezi Februari | NA                | NA           |
|   |                | Bei ya Mwezi Januari  | 1,721             | 1,721        |
|   |                | Mabadiliko (%)        |                   |              |
| TANGA   | TACACU         | Bei ya Mwezi Februari | 1,751             | 1,751        |
|   |                | Bei ya Mwezi Januari  | NA                | NA           |
|   |                | Mabadiliko (%)        |                   |              |

Ufunguo: NA = HAPO

Alama (    ) zinaonyesha mwelekeo wa mabadiliko ya bei. ( ) Bei imeongezeka; ( ) Bei imeshuka; ( ) Hakuna mabadiliko ya bei.

## 5.0 MKUTANO WA KIMATAIFA WA KOROSHO 2023

Tanzania ikiwa ni mojawapo ya nchi zinazoongoza kwa uzalishaji korosho duniani, huku ikishika nafasi ya pili katika bara la Afrika na nafasi ya sita duniani kwa mujibu wa taarifa za African Cashew Alliance (2021). Bodi ya Korosho Tanzania inatarajia kuratibu mkutano wa kimataifa wa korosho nchini utakaoitwa "Tanzania International Cashew Conference" kuanzia tarehe 11 Oktoba, 2023 hadi 14 Oktoba, 2023, katika ukumbi wa mikutano wa kimataifa wa Mwalimu Nyerere.

Lengo la mkutano huo ni kuhamasisha maendeleo ya zao la korosho kwa kutangaza fursa za uwekeza-ji zilizopo katika zao la korosho. Kupitia mkutano huo, inatarajiwa ushiriki wa wadau mbalimbali katika Nyanja za utafiti, utengenezaji mashine za usindikaji, viwanda vya ubanguaji na uwekezaji. Mkutano huo utaenda sambamba na maonyesho ya bidhaa zitokanazo na zao la korosho na teknolojia mbalimbali zitumikazo katika usindikaji wa bidhaa za korosho.

## 6.0 TAARIFA YA MINADA KWA MKOA YA TANGA, DODOMA NA SINGIDA

Msimu wa mavuno kwa mikoa ya kanda ya kati (Singida na Dodoma) na Kaskazini (Tanga) ikiwa ndio umeanza ambapo matarajio ya uzalishaji ni tani 2,000 kwa mkoa wa Tanga, tani 200 kwa mkoa wa Singida na tani 60 kwa mkoa wa Dodoma. Minada katika mkoa wa Tanga ilianza tarehe 1 Februari, 2023 ambapo kiasi cha tani 199.168 za korosho ghafi ziliuzwa

## 7.0 UBORA WA KOROSHO KWA MKOA WA PWANI MSIMU WA 2022/2023

Hali ya ubora wa korosho kwa mkoa wa Pwani umeendelea kuimarika ambapo katika msimu wa 2022/2023 asilimia 96 ya korosho ghafi zilizopokelewa kwenye ghala za mnada zilikuwa ni daraja la kwanza ikiwa ni ongezeko la 24% ukilinganisha na msimu wa 2021/2022 ambao ubora wa korosho daraja la kwanza ulikuwa 72%.

## 8.0 ZOEZI LA UHUISHAJI WA KANZIDATA YA WAKULIMA WA ZAO LA KOROSHO

Bodi ya korosho kwa kushirikiana na Halmashauri zinazolima zao la korosho inaendelea na zoezi la kuhuisha kanzi data ya wakulima wa korosho. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari tayari manispaa ya Mtwara Mikindani, Halmashauri ya wilaya ya Mtwara na Halmashauri ya wilaya Nanyamba zimehuisha kanzi data za wakulima. Zoezi bado linaendelea na mpaka sasa jumla ya wakulima 24,469 wamefikiwa na kuhuishwa taarifa zao katika halmashauri hizo tatu kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8 Taarifa ya Mwenendo wa Uhuishaji wa Kanzidata ya Wakulima wa zao la Korosho katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Manispaa ya Mtwara Mikindani na Halmashauri ya Wilaya Nanyamba.**

| Na. | Halmashauri                    | Idadi ya Wakulima Waliofikiwa |
|-----|--------------------------------|-------------------------------|
| 1   | Manispaa ya Mtwara             | 1,888.00                      |
| 2   | Halmashauri ya Wilaya Mtwara   | 12,833.00                     |
| 3   | Halmashauri ya Wilaya Nanyamba | 9,748.00                      |
|     | <b>Jumla</b>                   | <b>24,469.00</b>              |

## 9.0 ZOEZI LA USAMBAZAJI MBEGU BORA ZA KOROSHO MSIMU WA 2022/2023

Msimu wa mwaka 2022/2023 Bodi ya korosho ilipokea mahitaji ya kilo 25,780 sawa na tani 25.78 za mbegu bora za korosho kutoka katika Halmashauri mbalimbali nchini. Zoezi la usambazaji wa mbegu bora lilianza tangu tarehe 20/12/2022 na bado linaendelea ambapo jumla ya tani 20.512 zimeshasam-bazwa na tani 5.27 zipo kwenye hatua za mwisho za kusambazwa. Taarifa ya usambazaji kimkoa ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 9

### Jedwali Na. 9: Taarifa ya Usambazi Mbegu Bora za Korosho Kimkoa

| Mkoa             | Kiasi cha mbegu (Kg) | Zilizosambazwa | Zisizosambazwa |
|------------------|----------------------|----------------|----------------|
| MtWARA           | 560                  | 560            | 0              |
| LINDI            | 8,000                | 8,000          | 0              |
| PWANI            | 1,800                | 1,800          | 0              |
| TANGA            | 3,902                | 3,902          | 0              |
| KIGOMA           | 160                  | 160            | 0              |
| SHINYANGA        | 200                  | 0              | 200            |
| MBEYA            | 1,000                | 400            | 60             |
| SONGWE           | 1,000                | 0              | 1,000          |
| RUVUMA           | 3,173                | 460            | 2,713          |
| MOROGORO         | 5,390                | 5,390          | 0              |
| NJOMBE           | 595                  | 0              | 595            |
| <b>Jumla Kuu</b> | <b>25,780</b>        | <b>20,512</b>  | <b>5,268</b>   |

## 9.1 MICHE ITAKAYOZALISHWA NA KUSAMBAZWA

Kilo moja ya mbegu bora ya korosho inaweza kuzalisha miche 140 hivyo kwa mbegu kilo 25,780 zinazalisha jumla ya miche 3,609,200 itakayosambazwa bure kwenda kwa wakulima na kwenye mashamba ya pamoja yatakayoanzishwa kwenye Halmashauri. Miche hii inatosha kupandwa kwenye eneo la ekari 133,674.1.



Jarida hili limetolewa na;  
Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu,  
Bodi ya Korosho Tanzania.  
S.L.P 533  
MTWARA  
[info@cashew.go.tz](mailto:info@cashew.go.tz)